

**SUBSIDIARY LEGISLATION**

*to the Gazette of the United Republic of Tanzania No. 25 Vol. 103 dated 24<sup>th</sup> June, 2022  
Printed by the Government Printer, Dodoma by Order of Government*

TANGAZO LA SERIKALI NA. 457 la tarehe 24 /6/ 2022

**SHERIA YA UWAKALA WA MELI TANZANIA,  
(SURA YA 415)**

**AMRI**

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 28(3))*

AMRI YA NAULI ZA ABIRIA WA USAFIRI MAJINI ZILIZOREKEBIWA, 2022

- Jina 1. Amri hii itajulikana kama Amri ya Nauli za Abiria wa Usafiri Majini Zilizorekebiwa, 2022.
- Matumizi 2. Amri hii itatumika kwa meli za abiria zilizosajiliwa au  
Sura ya 165 kupewa leseni chini ya Sheria ya Usafiri Majini na kanuni zake wakati ikisafiri katika maeneo ya maji ya Tanzania.
- Tafsiri 3. Katika Amri hii, isipokuwa kama muktadha unahitaji  
vinginevyo-  
Sura ya 415 “Sheria” maana yake ni Sheria ya Uwakala wa Meli Tanzania;  
“nauli za rejea” maana yake ni nauli za abiria zilizotumika katika njia za ndani za usafiri majini kama zilivyokusanywa na Shirika mwezi Agosti, 2020;  
“Shirika” maana yake ni Shirika la Uwakala wa Meli Tanzania lililoanzishwa chini ya kifungu cha 4 cha Sheria;  
Sura ya 165 “meli iliyosajiliwa” maana yake ni meli yenye urefu wa angalau mita ishirini na nne iliyosajiliwa na Shirika kwa mujibu wa Sheria ya Usafiri Majini; na  
Sura ya 165 “chombo kidogo chenye leseni” maana yake ni meli yenye urefu usiofikia mita ishirini na nne iliyosajiliwa na Shirika

kwa mujibu wa Sheria ya Usafiri Majini.

Nauli  
zilizoidhinishwa  
kwa meli  
zilizosajiliwa

4. Mtu anayeendesha meli iliyosajiliwa atatumia nauli zilizoidhinishwa kama ifuatavyo:

- (a) nauli iliyorekebiwa ambayo si zaidi ya asilimia 32.5 juu ya nauli za rejea kwa meli hizo katika madaraja mbalimbali, kama yapo; na
- (b) nauli iliyorekebiwa na kukadiriwa kuwa sawa na elfu ya karibu ili kuwezesha biashara.

Nauli  
zilizoidhinishwa  
kwa chombo  
kidogo chenye  
leseni

5. Mtu anayeendesha chombo kidogo chenye leseni atatumia nauli zilizoidhinishwa kama ifuatavyo:

- (a) nauli iliyorekebiwa ambayo si zaidi ya asilimia 21.4 juu ya nauli za rejea za chombo hicho; na
- (b) nauli iliyorekebiwa na kukadiriwa kuwa sawa na miatano ya karibu ili kuwezesha biashara.

Shirika kutoa  
nauli  
zilizorekebishwa

6. Shirika litatangaza nauli iliyorekebiwa kwa mujibu wa Amri hii, kwa njia za ndani za usafiri majini ndani ya siku saba tangu tarehe ya kutangazwa kwa Amri hii.

Kuzingatia  
viwango vya  
usalama  
Sura ya 165

7. Mtu atakayetumia nauli zilizorekebishwa atazingatia viwango vya usalama kama vilivyotolewa na Sheria ya Usafiri Majini.

Dar es Salaam,  
17 Juni., 2022

KAIMU ABDI MKEYENGE  
*Mkurugenzi Mkuu*